



## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



Juni 12, 2023

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### Tamko la THBUB wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ajira kwa Watoto Juni 12, 2023

Tarehe 12 Juni ya kila mwaka ni **Siku ya Kimataifa ya Kupinga Utumikishwaji wa Mtoto Duniani – World Day against Child Labour**. Siku hii ilizinduliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka 2002 kama njia ya kuonyesha madhila wanayokutana nayo watoto wanaohusishwa katika ajira. Shirika la Kazi kupitia Mkataba wa Kimataifa Na. 138, liliweka umri wa ajira kuwa miaka 15 na kuendelea na katika Mkataba Na. 182 liliorodhesha ajira zisizokubalika kwa watoto na ambazo zinatakiwa kuzuiwa.

Tunapoadhimisha siku hii, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau mbalimbali wa haki za mtoto duniani katika kupinga ajira kwa watoto, sambamba na kuelimisha jamii juu ya madhara ya ajira hizo kupitia kauli mbiu ya mwaka huu isemayo: **“Haki ya Jamii kwa Wote. Kukomesha Ajira ya Watoto!”**

Tume inatambua na kuunga mkono juhudini mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kutokomeza ajira kwa watoto ikiwa ni pamoja na kuridhia

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA / Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz), [zanzibar@chragg.go.tz](mailto:zanzibar@chragg.go.tz); Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

Mikataba ya Kikanda na Kimataifa, kutunga Sera na Sheria ya Mtoto ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Zanzibar ambapo zinakataza mtoto kuhusishwa katika kazi yoyote itakayoweza kumsababishia madhara kiafya, kielimu, kiakili, kimwili na katika ukuaji wake.

Pamoja na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa, bado zipo changamoto kadhaa, ikiwemo watoto kuendelea kufanyishwa kazi ngumu katika maeneo ya kazi za ndani, mashambani, mitaani, na migodini. Ajira hizi zimekuwa kichocheo cha ukatili dhidi ya watoto ambapo baadhi yao hukosa masomo, kunyonywa kiuchumi kwa kuwa hulipwa ujira mdogo na matatizo ya kiafya, jambo linaloathiri ukuaji wao.

Miongoni mwa sababu zinazoendelea kuchangia ajira kwa watoto ni pamoja na umasikini na jamii kukosa uelewa juu ya madhara ya ajira hizo, hali inayopelekea watoto kufanya kazi ngumu ili kujikimu.

Kupitia kauli mbiu ya mwaka huu, THBUB inaendelea kuhamasisha jamii kuheshimu haki za binadamu katika masuala ya kazi na ajira, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria, Sera na Miongozo mbalimbali inayolinda haki za mtoto nchini. Pia, THBUB inatoa wito kwa Serikali, wadau na jamii kuunganisha nguvu kupinga ajira kwa watoto mahali popote nchini.

Pamoja na wito huo, THBUB inapendekeza yafuatayo:

1. Serikali iendelee kuhamasisha hatua za kimataifa kufikia haki ya kijamii na kuondoa ajira kwa watoto kama moja ya mambo yake muhimu;

2. Serikali iendelee kuhakikisha kuwa suala la kutokomeza tatizo la ajira kwa watoto linapewa kipaumbele katika utengenezaji wa sera, shughuli za kitaifa na kimataifa, katika ushirikiano wa maendeleo na katika mikataba ya kifedha, biashara na uwekezaji;
3. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iendelee kutoa elimu ya haki za mtoto na madhara ya ajira mbaya kwa watoto;
4. Jamii iendelee kutoa ushirikiano kwa kuwafichua watu wote wanaowaajiri na kuwatumikisha watoto; na
5. Wazazi na walezi wahakikishe wanawatunza, kuwalinda na kuwapatia watoto mahitaji yao ya msingi. Aidha, wahakikishe watoto wote wanahudhuria shule na hawatumii kama vitega uchumi vya familia kwa kuwafanyisha kazi ngumu, zisizofaa na zinazowaathiri.

***'Haki ya Jamii kwa Wote. Kukomesha Ajira ya Watoto!'***

Imetolewa na:



Mohamed Khamis Hamad  
**Makamu Mwenyekiti**

## **TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Juni 12, 2023